

*Rosi alichoshwa na hisia ya kutostahili kuwa wa mahala pale.*



# Sala ya Rosi

**Na Lucy Stevenson Ewell**  
(Imetokana na hadithi ya kweli)

Rosi alidondosha begi lake la Mngongoni sakafuni. Ndiyo kwanza alikuwa amemaliza siku yake ya pili katika darasa lake jipya. Na haikuwa siku nzuri.

"Kuna tatizo gani?" Mama aliuliza. Rosi alijibwaga kwenye kochi. "Baadhi ya watoto darasani kwanza walisema mambo mabaya juu yangu," alisema. "Kuhusu ngozi yangu ya kahawia."

Hawakuwepo watu wengi shule ni waliokuwa na ngozi yenyre rangi kama ya Rosi, kwa hiyo alihisi kama hakustahili kuwa pale. Lakini utani ulimfanya ahisi vibaya mara mia zaidi.

Mama alionekana mwenye wasiwasii. "Nasikitika," alisema. Alimkumbatia Rosi. "Nitaongea na mwalimu wako kuhusu hilo."

Lakini siku ya pili shulenii, Rosi alitaniwa tena. Mvulana mmoja

darasani kwake alimfanya mzaha siku nzima.

Rosi alihisi huzuni. Lakini pia alihisi hasira. Wakati mwengine mvulana huyo alipokoswa adabu, Rosi alibishana naye. Lakini hiyo haikumfanya ahisi vizuri.

Siku moja wakati Rosi aliporudi nyumbani kutoka shule, alikimbia moja kwa moja chumbani kwake. Alikuwa amechoka kufanyiwa

mzaha. Alichoka kuhisi hastahili kuwa pale. Alifunika uso wake kwa mto na alilia.

*Nitafanya nini?* aliwaza. Hakutaka kuhisi hivi kwa mwaka wote wa shule.

Rosi alifuta macho yake. Kisha aliangalia juu kwenye sanamu ndogo ya Yesu ambayo ilikuwa juu ya rafu ya vitabu vyake. Mama alikuwa amempa Rosi ili imsaide kumkumbuka Yesu.

*Labda napaswa kusali,* aliwaza. Alipiga magoti na kukunja mikono yake.

"Baba mpendwa wa Mbinguni," nina maumivu makali ndani yangu. Wanafunzi wenzangu wamekuwa wakatili kwangu kwa sababu ya ngozi yangu ya kahawia, na inanifanya nihisi vibaya. Tafadhalii nisaidie."

Ilikuwa vizuri kumweleza Baba wa Mbinguni kuhusu hisia zake. Alijua Alikuwa anasikiliza. Alihisi ukunjufu wa moyo na kupendwa, kama vile alikuwa anafunikwa na blanket laini. Alihisi kwamba rangi yake ya ngozi ilikuwa nzuri. Alikuwa mtoto wa Mungu, na Mungu alimpenda.

Wakati Rosi alipomaliza kusali, alikuwa amepata wazo. Labda kulikuwa na mengi zaidi ambayo angeweza kufanya ili kusaidia kwenye shule yake.

Wiki iliyofuata, Rosi na mama yake walizungumza na watu wenye madaraka katika shule kuhusu nini kilikuwa kinatokea katika darasa lake. Rosi aliwatafuta watoto wengine shulenii waliokuwa wanafanyiwa vitendo vya uonevu na alikuwa rafiki yao. Alijaribu kutomjali mvulana aliyekuwa anamfanya utani. Na kanisani siku ya Jumapili, alishiriki ushuhuda wake kwamba Baba wa Mbinguni alimpenda *kila mtu*.

Mambo shulenii hayakutengemaa mara moja. Lakini wakati yalipokuwa magumu, Rosi alikumbuka jinsi alivyohisi wakati wa sala yake. Yeye alikuwa mtoto wa Mungu, na Mungu alimpenda. Na kwa sababu alijua hivyo, angeweza kufanya chochote. ●



VIELEZO NA SHAWNA J. TENNEY



## MADOKEZYO YA ROSI YA KUNG'OA UBAGUZI WA RANGI

**UBAGUZI WA RANGI** ni wakati watu wanapotendewa kwa uonevu kwa sababu ya rangi ya ngozi yao au asili yao. Hapa ni mambo unayoweza kufanya:

- Kumbuka kwamba wewe ni mtoto wa Mungu.
- Mtendee kila mtu kwa upendo, ukarimu na heshima. Kumbuka kwamba wao ni watoto wa Mungu pia.
- Kama unaonewa au kama unaona mtu fulani anaonewa, zungumza na mtu mzima. Jitetee, lakini usioneshe hisia na ukatili ule ule ambao umeoneshwa kwako.
- Shiriki uzoefu wako na wengine. Wasaidie wajue kwamba hawako peke yao.
- Watetee wengine wanaonetndewa isivyo sahihi. Kuwa rafiki yao.